MAADHIMISHO SIKU YA UKIMWI DUNIANI

# Bado juhudi zinahitajika kupambana na maambukizi mapya

## ► Vijana sasa waongoza kwa maambukizi

NA MOHAMMED SHARKSY, SUZA

**KESHO Disemba 1 ni siku ya Ukimwi duniani ambapo Zanzibar kama sehemu ya dunia nayo itaadhimisha siku hiyo.**

**Makamu wa pili wa Rais Hemed Suleiman Abdulla, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika hafla ambayo itafanyika ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul Wakili ulipo Kikwajuni Mjini Unguja.**




Tuvishinde Vikwazo vya Fedha, Tuimarishe Mapambano ya UKIMWI", ndio kauli mbiu yam waka 2025, ambayo inaakisi kuwepo changamoto ya upungufu wa fedha za kuendeleza mipango ya kudhibiti Ukimwi baada ya wahisani wengi kupunguza misaada yao kwa ajili ya kusaidia mapambano dhidi ya ukimwi.

Kauli mbiu ya dunia mwaka huu inasema "Kujikomboa kutoka kwenye matatizo, kubadilisha namna ya kukabiliana na UKIMWI, huku Tanzania, ikija na kaulimbiu ya "Mapambano dhidi ya UKIMWI ni wajibu wa kila mmoja. Tuwajibike, tuelimike, tupime afya zetu na tuwafikie walio hatarini zaidi. Kwa pamoja tunaweza kufikia kizazi kisicho na UKIMWI."

Kutokana na mijumbe hiyo dunia na Tanzania kwa ujumla zimefika wakati kuondokana na changamoto za kifedha, kijamii na kimfumo ambazo zimekuwa zikikwamisha kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo na hasa kutegemea wahisani kutoka nje.

Kimantiki siku hii ni muhimu ya kutafakari na kukumbuka changamoto zinazosababishwa na UKIMWI, kuenzi walio katika matibabu na kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya maambukizi mapya.

Ikiwa miongo kadhaa imepita tangu kugundulika kwa ugonjwa huu, bado dunia inaendelea kutafuta mbinu mpya za kupunguza maambukizi mapya, kuimarisha huduma na kuhakikisha tiba dhidi ya visuri vya UKIMWI inapatikana bila vikwazo.

Aidha, inatukumbusha kwamba dunia inabadilika na hivyo mbinu za kupambana na UKIMWI lazima zibadilike hasa katika matumizi ya teknolojia, ushirikiano mpana, na uwekezaji wa ndani.

**HISTORIA YA UKIMWI ZANZIBAR**

Historia ya visiwa vya Zanzibar inaeleza kuwa ugonjwa huo uligundulika mwaka 1986 ambapo kesi tatu za kwanza ziligundulika katika hospitali ya Rufaa Mnazimmoja.

Baada ya kujitokeza hali hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukua hatua ya kuanzisha kitengo maalum cha Ukimwi chini ya Wizara ya Afya na kupewa jukumu la kuhakikisha maradhi hayo yanadhibitiwa hapa Zanzibar na hayawi tatizo katika jamii.

Tume ya Ukimwi ilianzishwa mwaka 2002 kwa lengo la kuratibu shughuli zote zinazohusu Ukimwi.

Kwa Zanzibar maeneo yanayoongoza na maambukizi ya VVU kwa Unguja ni Mkoa wa Mjini Magharibi na kisiwa cha Pemba ni wilaya ya Wete.

**HALI YA UKIMWI DUNIANI – 2024/2025**

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Kukabiliana na UKIMWI (UNAIDS) za mwaka 2024/2025, dunia imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na ugonjwa huo, lakini bado ipo mbali na lengo la kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030.

Takwimu zinaonesha zaidi ya watu milioni 38.4 wanaishi na VVU, ambapo kwa mwaka 2024 pekee kulikuwa na maambukizi mapya milioni 1.3, huku vifo vilivyotokana na UKIMWI vikifikia 650,000.

Aidha, takwimu hizo zinaonesha zaidi ya watu milioni 28.7 wanatumia dawa za kufubaza vizusi vya (ARVs).

**HALI YA UKIMWI TANZANIA**

Tanzania, chini ya Tume ya Kukabiliana na UKIMWI (TACAIDS) na Wizara ya Afya, kuna hatua za msingi zilizopigwa katika kupunguza maambukizi mapya, kuongeza upimaji na kuimarisha upatikanaji wa dawa.

Kwa mfano, ripoti ya TACAIDS zinaonesha idadi ya watu wazima wanaoishi na VVU imefikia asilimia 4.4.

Aidha, ripoti inaonesha kuwa ni asilimia 82.7 ya waliopima wanajua hali zao na asilimia 97.9 kati yao, wanatumia ARVs.

Pia asilimia 94.3 ya wanaotumia ARVs wamefikia kiwango cha kukandamiza makali ya virusi (Viral Load Suppression), hii imeifanya Tanzania kukaribia kufikia lengo la "95-95-95" la UNAIDS.

**HALI YA UKIMWI ZANZIBAR**

Kwa mujibu wa takwimu za ukimwi Zanzibar inaonesha kutoshuka ama kupanda kwa wagonjwa wa ukimwi ambapo inaonesha ni asilimia 0.4.

Hali ya ukimwi Zanzibar inaonesha kuwa bado inapambana na maumbukizi mapya kwa kuwa imeendelea kudhibiti maambukizi ya VVU, ikiwa na kiwango cha chini zaidi cha maambukizi katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Takwimu rasmi za mwaka 2025, zinaonesha kiwango cha maambukizi ni 0.4% ambapo watu wanaoishi na VVU ni takribani 10,256.

Aidha, kuna watu 9,842 wanaotumia ARVs – sawa na 96% ya wanaohitaji matibabu.

**MAKUNDI YANAYOONGOZA KWA MAAMBUKIZI**

Takwimu zinaonesha watu wenye umri miaka 45 na zaidi ndio wanaoongoza kwa maambukizi huku wanawake wakiwa ni mara mbili zaidi ya wanaume katika maambukizi.

Aidha, wanawake wanaofanya biashara ya ngono wako kwenye maambukizi kwa 21.1% wakifuatiwa na wanaume wanaojamiiana, ambao ni asilimia 11.4% wakati watumiaji wa dawa za kulevya kwa kujidunga ni 9.3%.

**MIKAKATI YA SERIKALI KUPAMBANA NA UKIMWI**

Pamoja na yote hayo, Zanzibar inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 tatizo la ukimwi liwe limepungua am kumalizika kabisa.

Ili kufikia shabaha hizo pia zipo shabaha nyengine ni kuona asilimia 95 ya watu wanaoishi na VVU ifikapo mwaka 2030 wawe wanajitambua, 95 ya pili ya wale wanaoishi na VVU wanatumia dawa za kupunguza makali ya VVU na 95 ya tatu ifikapo mwaka huo wanaotumia dawa za ARV wawe wameweza kufubaza virusi vya Ukimwi ndani ya miili hayo.

Ikiwezekana kuzifikia shabaha hizo kuna uwezekano mkubwa wa kufikia lengo la mwaka 2030ni wazi kuwa maradhi ya ukimwi yanaweza kupungua ama kumalizika.

**CHANGAMOTO**

Licha ya mafanikio yanayopatikana katika mapambano dhidi ya UKIMWI, bado zipo changamoto zinazorudisha nyuma juhudi hizo.

Miongoni mwa changamoto hizo ni uelewa mdogo kwa vijana kuhusu virusi vya UKIMWI, kupungua kwa rasilimali kutoka kwa washirika wa maendeleo na mahitaji ya kuunganisha huduma za VVU na huduma nyingine.

Changamoto kubwa kwa Zanzibar watu kupata maambukizo ya virusi vya Ukimwi wanalihusisha na zinaa kwa utamaduni wetu, dini mtu ambayo hutoa sura mbaya katika jamii.

Licha ya juhudi kadhaa kuchukuliwa na UKIMWI kuwa mtambuka katika jamii lakini bado unyanyapaa upo jambo ambalo hata wanao maambukizi wanashindwa kujieleza bayana.

**MAFANIKIO**

Mafanikio ni mengi sana ukilinganisha na miaka ya nyuma na kwamba unyanyapaa umepungua kwa kiasi fulani, jamii imekuwa mtambuka.

Maambukizi ya mama wajawazito bado yako chini ya asilimia 1 kwa kuwa Shirika la Afya duniani linataka kuona nchi inapunguza maambukizi ya mama kwenda kwa mtoto angalau yawe kwa asilimia 2.5.

Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi wanaendelea kumeza dawa kama wanavyoelekezwa na daktari ili kushusha virusi vyao.

**NINI KIFANYIKE**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TACAIDS na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamisheni ya UKIMWI (ZAC), zimetangaza dhamira ya kuendelea kuwekeza katika elimu kwa jamii, upimaji wa hiari na ushauri, uduma jumuishi za VVU, matibabu endelevu ya ARVs kwa wanaoishi na ugonjwa huo na kupinga unyanyapaa na ubaguzi.

**HITIMISHO**

Siku ya UKIMWI Duniani 2025 si tu kumbukumbu; ni mwito wa mabadiliko na hatua.

Ni wito wa kutumia sayansi, teknolojia na mshikamano wa kijamii kuhakikisha kizazi kijacho hakikabiliwi tena na maumivu ya UKIMWI ambayo yamepoteza maisha ya mamilioni ya watu, yanaendelea kuathiri nguvu kazi na kuacha familia nyingi zikilea mayatima.

Kwa pamoja, tunaweza kufikia jamii isiyo na maambukizi mapya, isiyo na vifo vitokanavyo na UKIMWI, na isiyo na unyanyapaa.




